Changamoto ya Biblia kwa Maaskofu

-Na Mch. Marek P. Zabriskie, Mchungaji Kiongozi wa Kanisa la Mt. Thomasi la Fort Washington, PA, Mwanzilishi wa Kituo cha Masomo ya Biblia na Changamoto ya Biblia
www.thecenterforbiblicalstudies.org

Mmoja wa Mababa wa Kanisa aliandika, "Jinsi askofu anavyoenenda ndivyo na dayosisi inavyoenenda." Muonekano na mfano wa askofu unaweza kuwagusa maelfu ya watu katika kukua kiroho.

Tafiti zinaonyesha kuwa njia ya kwanza kubwa ya kutukuza kufikia utu uzima wa kiroho kama Wakristo ni kwa kusoma Maandiko kila siku. Kusikiliza maandiko yakisomwa kanisani ni sawa na kukaa kwenye kiti cha abiria cha gari. Hatujifunzi jinsi ya kuendesha gari au kujifunza njia ya tuendako.

Kituo cha Masomo ya Biblia (*CBS – Centre for Biblical Studies*) kinamhimiza kila askofu kuwaalika makasisi na walei wa dayosisi yake kumuunga mkono askofu katika kusoma Biblia yote kwa mwaka mmoja kwa lengo kuu la kuwasaidia maelfu ya watu kuanzisha tabia ya maisha yote ya kusoma Biblia kila siku.

Tafiti zimeonyesha kuwa kama mtu atasoma Biblia kwa siku 21 kwa mfululizo ana uwezekano wa 80% wa kuanzisha nidhamu ya maisha yake yote ya kusoma Biblia kila siku na usomaji huo wa Biblia mara nne au zaidi kwa wiki utaleta mabadiliko chanya yanayopimika katika tabia ya uadilifu.

Ili kuwasaidia maaskofu, tunapendekeza mambo yafuatayo:

Muda Muafaka

Dayosisi yako na wewe mnaweza kuanza Changamoto ya Biblia wakati wowote katika mwaka.

Tumegundua kuwa nyakati za kufaa zinaweza kuwa pamoja na:

Anza Januari 1, wakati watu wengi wanafanya Maazimio ya Mwaka Mpya. Wahimize makasisi na walei kuungana nawe katika kufanya azimio la kiroho kwa kusoma Biblia pamoja nawe wakifuata taratibu ya masomo ya mwaka.

Anza wakati wa Kwaresma ana tumia Changamoto ya Biblia kama nidhamu yako ya Kwaresma na endelea nayo mwaka mzima.

Anza mwanzoni wa msimu wa Kiangazi wakati watu wengi hawana shughuli nyingi na wana muda zaidi wa kusoma.

Anza wakati wa kipupwe, kuanzia mwezi wa Septemba hadi Agosti.

Anza wakati wa Maajilio ili kusoma Maandiko kwa mwaka wote wa Kanisa.

Zondervan hutoa changamoto ya siku 90 ya kusoma Biblia yote, lakini mpango huu wa muda mfupi ni mgumu kwa wasomaji wengi au watu wenye shughuli nyingi. Tunapendelea ufuate usomaji wa taratibu, wenye tafakari zaidi ya usomaji wa Biblia.

Tafsiri

Tunapendekeza kwa msomaji wa Kiingereza usome *New Oxford Annotated Edition* [kwa msomaji wa Kiswahili usome *The Holy Bible in Kiswahili Union Version with Concordance 1997*]

Kasi ya Usomaji

Tunakuhimiza kuwaalika makasisi na walei: 1) kusoma sura za Agano la Kale, 2) zaburi moja na 3) sura moja ya Agano Jipya kila siku. Hii itakuwaidia kupitia Biblia yote kwa mwaka.

Mbinu hii hupelekea usomaji wenye mafanikio wa vitabu vya Biblia kwa mtiririko, na hutoa unafuu kuwasaidia wale wanaosoma sehemu zisizovutia za Maandiko ya Kiebrania.

Kutumia Teknolojia na Kugawa Biblia

Tunapendekeza makasisi na walei wa dayosisi yako kufikiria kuchapua Biblia katika iPad, iPhone, Kindle, Nook au vifaa vingine vya kielekroniki, na kusikiliza kwenye CDs. Biblia ya NIV tayari ipo kwenye CDs.

Tunapendekeza kuwa utoa Biblia za bure kwa wale wasio kuwa nazo.

Kuwafikia Wengine

Tunawahimiza maaskofu kuwafikia marafiki na wale walio na uhusiano nao katika dayosisi zao na nje ya dayosisi kujiunga nao katika usomaji wa Biblia kwa mwaka, wakiwemo wanafunzi wa uchungaji na wote wanaoandaliwa kwa huduma ya uchungaji.

Wewe ndiye muinjilisti wa kwanza katika dayosisi. Tunakuhimiza kuongoza kwa mfano na kuwatia moyo makasisi kutenda vivyo hivyo katika mitaa yao.

Washirikishe shuhuda katika vipeperushi vya dayosisi katika ziara za kidayosisi na makongamano jinsi Changamoto ya Biblia inavyokubadilisha wewe na wengine.

Wafahamishe ikiwa mwenzio unayekaa naye chumba kimoja chuoni amekubali mwaliko wako wa kusoma Biblia pamoja nawe.

Kuwashirikisha Wengine Uzoefu Uletao Mabadililo wa Changamoto ya Biblia

Washirikishe shuhuda katika kipeperushi cha dayosisi, ziara za pareshini na kwenye mikutano ya dayosisi jinsi Changamoto ya Biblia inavyokubadilisha wenwe mwenyewe na wengine.

Washirikishe wengine katika dayosisi yako kile unachogundua kadri unavyosoma Biblia yote tena na tena.

Jadili sehemu za Biblia zisizopatikana katika Taratibu ya Masomo.

Wasaidie wengine katika dayosisi kuifahamu changamoto ya kuelewa sehemu za Biblia zinazomuhusisha Mungua na vurugu na mateso.

Tovuti ya CBS inatoa makala za Profesa Walter Brueggemann kuhusu masuala haya, ambazo ni hazina nzuri kwa vikundi vya kujisomea Biblia katika dayosisi.

Mbinu Zilizopendekezwa za Usomaji

Wape ruhusa wale wanaoshiriki katika Changamoto ya Biblia kuruka au kupitia kwa haraka nasaba na sheria za vyakula, ili wasicheleweshwe kufikia lengo lao la kusoma Biblia yote.

Kuanzia 2012 tovuti ya CBS itatoa mpango wa mwaka mmoja wa usomaji wa Biblia. Kutakuwa na tafakari ya usomaji wa kila siku, swali na sala zinazoendana na masomo ya kila siku, zilizoandikwa na maaskofu, makasisi, walezi wa vyuo vya uchungaji, waandishi na wanazuoni.

Tunatetea mbinu ya kiroho na siyo ya kiakili tu na kitaaluma ya usomaji wa Biblia. Kila msomaji ajiweke katika uwepo wa Mungu kabla ya kusoma.

Tunaipenda kawaida ya watawa wa zamani ya *lectio divina*, ambapo wasomaji husoma kifungu, hukitafakari, huomba kwa Mungu na kukaa kimya kusikiliza majibu ya Mungu – yaani *lectio*, *meditation*, *oratio* na *contemplatio*. Wahimize wale wanaosoma Biblia pamoja nawe kutulia kwa muda na kuomba wakati wa kusoma au baada ya kusoma.

Tovuti yetu *www.thecenterforbiblicalstudies.org* inatoa msaada mkubwa kuwasaidia waumini katika dayosisi yako na wewe mwenyewe.

Jinsi ya Kukuza Changamoto ya Biblia katika Kanisa lako na Nje ya Mipaka Yake

Tunapendekeza kuwaandikia makasisi wote na kuweka makala kwenye vipeperushi vya dayosisi ili kuialika dayosisi yote kujiunga katika kusoma Biblia yote kwa mwaka mmoja.

Muombe kila kasisi kiongozi kutangaza mwaliko wako wa kujiunga kwenye Changamoto ya Biblia katika vipeperushi vya mtaa na matangazo ya Jumapili.

Jaribu kutumia matangazo kwenye magazeti kuwaalika kuwaalika wana jamii kujiunga na dayosisi yako na wewe mwenyewe katika Changamoto ya Biblia.

Waombe makasisi wako kufanya jitihada za matamasha ili kuwaalika watu wengine nje ya makanisa yao kujiunga na Changamoto ya Biblia.

Kutwaa Fursa ya Kujitangaza Bure

Tunahimiza kuviarifu vyombo vya habari kufahamu kwamba wewe na dayosisi yako mnashiriki katika Changamoto ya Biblia.

Jaribu kuandika makala katika gazeti kuhusu Changamoto yako ya Biblia. Kwa kuwa Waanglikana hawafahamika kama wasomaji wa Biblia wenye nguvu, tumeona mutikio mkubwa wenye upendeleo wa vyombo vya habari kuhusu Changamoto ya Biblia.

Kila mwezi muombe muumini mmoja katika dayosisi aandike makala moja kwa ajili ya kipeperushi au gazeti lenu akieleza uzoefu alioupata wa kusoma Biblia na jinsi inavyombadilisha.

Kuwafikia Rika Zote

Tunapendekeza wazazi kusoma: *The Big Picture Story Bible* cha Scripture Union kwa watoto wenye umri wa miaka 2-7, *The Spark Bible* cha NRSV au DK Bible kwa watoto wenye umri mkubwa zaidi.

Kwa taarifa zaidi tembelea tovuti ya CBS ili upate "vichapisho kwa ajili ya watoto, vijana na familia." Tunawahimiza vijana katika dayosisi walio kuwa kiimani kujiunga na Changamoto ya Biblia wakitumia *NIV Teen Study Bible* kwa wasomaji wa Kiingereza [au Biblia itakayopendekezwa na Chama cha Biblia Tanzania, kwa wasomaji wa Kiswahili].

Tunashauri wale wasio na uhakika na imani yao wasome Agano Jipya kwanza kabla hawajaribu kusoma Biblia yote.

Pia tunashauri makundi ya vijana kanisani yaalikwe kusoma na kujadili Injili moja kila mwaka pamoja na kitabu kingine cha Biblia.

Kutoa Msaada wa Ushirikiano Endelevu

Ni muhimu kutoa msaada endelevu, na kuwafanya wawajibike na kuwasaidia, hasa wakati wa miezi mitatu ya kwanza ya Changamoto ya Biblia. Wale watakao kutana na mafanikio katika siku 90 za mwanzo wana uwezekano wa kusoma Biblia yote.

Hizi ndizo wiki ngumu wakati wasomaji wapya wa Biblia wanapogundua masimulizi yenye changamoto ambayo huwa hayasomwi kanisani.

Makanisa yanaweza kutoa vipindi endelevu ili kuwasaidia washiriki wa Changamoto ya Biblia katika siku zao za 90 za mwanzoni. Makanisa mengine huita vikundi hivi "Majadiliano ya Kina Kuhusu Biblia" au "Klabu ya Kitabu Kizuri".

Kujenga Moyo wa Uwajibikaji na Kutoa Msaada.

Tunapendekeza uchapishaji wa majina ya kila mtu anayeshiriki kwenye Changamoto ya Biblia kwenye kipeperushi cha dayosisi.

Jambo hili litafanya wengine wajue ni akina nani na ni wangapi wanaoshiriki. Jambo hili linaadhimisha moyo wao wa kujitoa na kuwafanya wawajibike katika kujitoa kwao.

Washiriki watawafahamu wengine wanaoshiriki katika Changamoto ya Biblia na hivyo kuwatafuta ili kuijadili Biblia.

Tunashauri yakusanywe majina na anuani za barua-pepe za wote wanaoshiriki katika Changamoto ya Biblia ili wewe kama askofu wao uzitumie kuwasiliana nao mara kwa mara au kwa njia yoyote kuwatumia ujumbe wa mara kwa mara wa kuwatia moyo na kuwapa neno la hekima washiriki.

Wasomaji wengi wamegundua kuwa mawasiliano haya ya mara kwa mara yamewatia moyo kufikia malengo yao. Barua pepe itakuwaidia wewe kutoa ufafanuzi maalumu kuhusu Biblia. Kwa kuwashirikisha jinsi Biblia inavyo imarisha imani yako, unaweza kuwatia moyo zaidi.

Tunahimiza kuwa maaskofu mara kwa mara maaskofu watume barua pepe binafsi kwa wachungaji ambao mitaa yao inashiriki kwenye Changamoto ya Biblia ili kuwapa ushirikiano.

Jambo hili litaanzisha mazungumzo ya mara kwa mara kwa njia ya mtandao kati ya maaskofu na makasisi kuhusu Biblia na Mungu, jambo ambalo hushirikishana mara chache uso kwa uso.

Uyahimize makanisa yanayoshiriki kuombeana kila Jumapili kwa ajili ya mabadiliko ya kiroho kwa wale wanaoshiriki Changamoto ya Biblia, na kumtaja aghalabu mshiriki mmoja katika sala Jumapili.

Hubiri kuhusu umuhimu wa kusoma Biblia unapofanya ziara za makanisa pareshini.

Kusherehekea Mafanikio ya Dayosisi Yako

Mwisho wa mwaka, maaskofu wanahimizwa kuandaa chakula cha hisani kwa wale wote walioshiriki katika Changamoto ya Biblia.

Tunapendekeza uzungumze katika hafla hiyo au umualike mwingine kuzungumzia baraka ya kiroho ya kusoma Biblia kila siku.

Makasisi na walei wanaweza kutoa ushuhuda mfupi jinsi usomaji wa Biblia ulivyowabadilisha maisha yao.

Toa hati ya kumtambua kila mtu aliyeshiriki kwa uaminifu katika kusoma biblia, na tuzo maalumu kwa wale walisoma Biblia yote

Kuzindua Upya Changamoto ya Biblia Katika Dayosisi Yako

Makasisi na walei waliosoma Biblia yote watoe shuhuda katika mikutano ya Dayosisi na katika mikusanyiko mingine ya dayosisi wakieleza jinsi usomaji wa Biblia ulivyobadilisha maisha yao.

Yatie moyo makanisa yanayoshiriki kuendesha madarasa ya ufuatiliaji kwa wale waliosoma Biblia yote na wale waliohangaika na hawakumaliza. Makundi yote mawili yatakuwa na maswali zaidi na njaa ya kujifunza Biblia.

Waalike wale waliosoma Biblia yote kuwa wasimamizi wa wale wanaosoma kwa mwaka wa pili.

Watie moyo wale waliosoma Biblia yote kujiunga na Elimu kwa Huduma (yaani *EFM – Education for Ministry*), ambayo ni hatua muhimu baada ya Changamoto ya Biblia.

Kutoa Uhiari wa Kuchagua na Kuzindua Changamoto ya Biblia katika Mwaka wa Pili

Zindua upya Changamoto ya Biblia kila mwaka ili kupata waumini zaidi katika dayosisi wasome Biblia yote.

Katika Mwaka wa Pili toa uhuru zaidi wa kuchaguzi kwa washiriki:

- Soma Biblia yote na Askofu
- Soma Agano Jipya na Askofu
- Soma Zaburi katika Kwaresma na Askofu
- Soma Injili Moja na Askofu

Soma Kitabu cha Matendo na Askofu

Jaribu kutumia mpango wa E100 uliyotolewa na Umoja wa Kujisomea Biblia (yaani Scripture Union). Mpango huu unaweka wazi vifungu 100 vya Biblia vinavyoeleza historia ya wokovu.

Jiunge na Askofu wako katika kuwa sehemu ya Mtaala wa Biblia wa Nyumbani.

Soma *The Message* cha Eugene Petersen (anayeweka Agano Jipya, Zaburi na Mithali katika lugha na fikra za kawaida)

Soma *The Story* cha Zondervan (masimulizi mfululizo ya Biblia, yanayoacha kando nasaba, na kanuni za vyakula, nk). Kimetengenezwa mahususi kwa wasomaji wapya.

Waalike wale waliosoma Biblia pamoja nawe katika tafsiri moja kuisoma tena pamoja nawe katika Mwaka wa Pili kwa kutumia tafsiri tofauti..

Kuzindua upya Changamoto ya Biblia inathibitisha kwamba lengo ni kuwa msomaji wa Biblia wa kila siku kwa maisha yote.

Kujenga Juu ya Mafanikio Yako katika Mwaka wa Tatu na Kuendelea

Waalike wale waliosoma sehemu ndogo za Biblia pamoja nawe (Agano Jipya, Zaburi au Injili) kuchukua changamoto kubwa zaidi mwaka unaofuata.

Mbeleni baada ya kustaafu, jambo la muhimu kuliko yote utakalokuwa umefanya kwa waumini wa dayosisi yako ni kuwashirikisha Neno la Mungu, lilipandwa ndani zaidi katika myoyo yao, na kuwatia moyo zaidi kusoma Biblia kila siku kwa maisha yao yote.

Mungu akubariki katika huduma yako na katika kazi muhimu ya kushirikisha wengine Neno la Mungu.

Nakushukuru kwa uongozi wako,

Marek

Waliomo katika Bodi yetu ya Washauri:

Askofu Mkuu Rowan Williams
Askofu Kenneth Kearon
Askofu James Tengatenga
Askofu Musonda Mwamba
Askofu David Moxon
Askofu Peter Carnley
Askofu Philip Poole
Askofu Frank Griswold
Askofu Mark Sisk
Askofu Wayne Wright
Askofu Peter James Lee
Askofu John Chane
Askofu Andy Doyle

Askofu Greg Rickel
Askofu Kirk Smith
Askofu Wayne Smith
Dkt. C.K. Robertson
Dkt. Harry Attridge
Mh. Mch. Dkt. Ian Markham
Mh. Mch. Dkt.Doug Travis
Dkt. Marcus Borg
Prof. Walter Brueggemann
Ndg Deirdre Good
Prof. Miroslav Volf
Mch. Scott Gunn
Mch. Simon Barnes
Ndg. Brian McLaren
Ndg. Phyllis Tickle
Mh. Mch. Sam Candler
Mh. Mch. Spenser Simrill
Mch. Carol Anderson

"Changamoto ya Biblia ni njia ya Kianglikana sana inayo fikirika na nyepesi ya 'kusoma, kuzingatia, kujifunza na kumeng'enya kwa ndani urithi wenye utajiri wa Maandiko Matakatifu. Tunaposherehekea mwaka huu wa 400 wa tafsiri ya Biblia ya King James, ambayo ni zawadi kubwa ya Waanglikana iliyogusa sana ulimwengu unaozungumza Kiingereza, Napendekeza Changamoto ya Biblia kama njia ya uhakika ya kuongeza uwezo wa kusoma Biblia miongoni mwa watu wetu."

Askofu Peter James Lee, Askofu Mtaafu wa Virginia

"Kituo cha Masomo ya Biblia kinatoa matumaini na zana kwa Kanisa letu. Kusoma Maandiko ni sehemu muhimu ya kanuni ya maisha ya Kanisa la Marekani na kumebadilisha maisha ya taifa letu katika nyakati ngumu na kutia moyo jitihada za utume wa Kanisa. Kwa kadri Kanis letu linavyotafuta kwenda katika utume, siku zote ni muhimu kwanza kujifanyia uinjilisti sisi wenyewe. Taratibu za usomaji wa Biblia kwa njia ya CBS zinatusaidia siyo tu kusoma Maandiko katika jamii bali pia kuiandaa jamii kwa ajili ya utume. Sisi sote tuna kanuni zetu ndani ya kanuni ya Maandiko, yaani sehemu zile tunazopendelea sana katika Maandiko. Kwa mfano wengi wetu tunaweza kusema kwa kichwa Yohana 3:16. Lakini tunaijua Yohana 3:17? 'Maana Mungu hakumtuma Mwana ulimwenguni ili auhukumu ulimwengu'. Kusoma kifungu chote ni kanuni ya Kianglikana ambayo inahakikisha kuwa sisi kama mtu mmoja mmoja siku sote tunaweka maisha yetu mbele ya maandiko na kutafuta kila mtu kubadilishwa kupitia Neno kabla hatujawaongoza wengine katika kugundua maisha yao ndani habari ya upendo wa Mungu uokoao."

Askofu Andy Doyle, Askofu wa Texas

"Changamoto ya Biblia ndicho kitu ambacho makanisa makuu ya USA yanahitaji kukipata katika njia yenye afya na yenye kuzaa matunda. Ni njia inayowapa nafasi wale wanaotembelea, wanaosali na waliowaumini wa makanisa yetu kugundua furaha ya kiroho toka katika masomo ya Biblia ya kila siku na katika uelewa wa ndani wa Neno la Mungu. Tunapanga kuyatia moyo makanisa yetu, wachungaji na walei katika Dayosisi ya Arizona kushiriki katika Changamoto ya Biblia ili wasome Biblia kwa manufaa na kuanzisha tabia ya kiroho ya kusoma Biblia kila siku kwa maisha yao yote. Napendekeza Changamoto ya Biblia kwa ajili ya Dayosisi yako, kanisa na wewe mwenyewe."

Askofu Kirk Smith, Askofu wa Dayosisi ya Arizona

"Mradi huu wa kusoma Biblia una umuhimu mkubwa sana kwa kanisa, kwa imani yake na kwa uhai wa utume wake. Katika nyakati hizi zenye mikanganyiko ya kiutamaduni na mashaka, kutilia maanani na kurudisha mapokeo ya kibiblia ni jambo muhimu. Ninashangilia njinsi watu walivyotayari, wenye nia na wanaweza kutumia maandiko haya ya kale yanayokwenda mbele ya matazamio yetu. Natazamia kuwa matunda mengi kwa ajili ya uaminifu wa kanisa yatazaliwa kutokana na kusoma Biblia pamoja."

Dkt. Walter Brueggemann, Profesa Mstaafu wa Seminari ya Theologia ya Columbia

"Kama ilivyo katika majadiliano yoyote yanayofaa, huchukua muda na nidhamu binafsi kusikiliza – kusikiliza kwa hakika – kwa lile Mungu analosema nasi kupitia Maandiko Matakatifu. Changamoto ya Biblia inatusaidia kufanya mazungumzo na Mungu, na kukua kiroho kunakotokana na mazungumzo hayo. "

Mch. C. K. Robertson, Shahada ya Uzamivu, Canon wa Askofu Mkuu wa Kanisa la Marekani

"Hakuna kilicho cha muhimu zaidi kwa Mkristo kuliko kusoma Maandiko kwa karibu na kwa uangalifu. Kituo cha Masomo ya Biblia na Changamoto ya Biblia vinataka kulibadilisha Kanisa; badala ya kuwa na Kanisa linalopuuza Maandiko, Kituo kinataka tuwe na Kanisa linalopenda na kujishibisha Maandiko. Jambo hili ni muhimu. Basi na turudishe tena usomaji wa Biblia na kwa hivyo kurejesha uaminifu."

Mch. Kiongozi wa Kanisa Kuu. Ian Markham, Mlezi wa Seminari ya Theologia ya Virginia

"Kama Askofu, ninasumbuliwa sana na tabia ya kutosoma Biblia ambayo ipo katika Kanisa. Nitapata mashaka kwamba Kanisa la Kiepiskopo linaelekea 'kuitelekeza' Biblia na usomaji wake wa makini, na kuiacha kwenye tafsiri na theologia ambazo hazileti taswira ya mapokeo yetu au ufahamu wetu. Changamoto ya Biblia, kwangu mimi, ni mwanzo mzuri, uliyo chanya na makini. Unaotambua tatizo halisi na kutoa mpango halisi na msaada wa kutatua tatizo hilo. Kwa nyongeza, naithamini sana ile hamu ya kusoma na kujifunza Biblia kuwa ni 'tabia ya kiroho ya maisha yote'. Nitaitia moyo dayosisi yetu kushiriki na kuwashukuru wale waliofanya mpango huu uwepo!"

Askofu Greg Rickel, Askofu wa Dayosisi ya Olympia

"Changamoto ya Biblia ni njia ambayo tumeihitaji na kuitamani kwa muda mrefu kwa ajili ya mitaa yetu na waumini wake ili kushiriki katika kusoma Biblia. Kusoma Biblia yamekuwa matazamia yenye changamoto kwa watu wengi na hivyo Kituo cha Masomo ya Biblia kinatoa njia kwa ajili ya kuleta mabadiliko hayo. Haitasaidia isipokuwa umefanya kile ambacho mtaala wa Biblia hufanya – kuleta maisha na nguvu mpya kwa kila Mkristo na kwa utume wa Kanisa. Hii ni kazi ya Roho Mtakatifu ambayo yafaa tuikaribishe."

Mch. Carol Anderson, aliyekuwa Mch. Kiongozi wa Kanisa la Watakatifu Wote, Beverly Hills

St. Thomas' Church
WHITEMARSH
Come with us on a journey with Christ

Bethlehem Pike and Camp Hill Road
Fort Washington, PA 19034
215-233-3970
stthomaswhitemarsh.org